

# UPONYAJI MTAKATIFU WA KISASA.

## I. Utangulizi:

1. Uponyaji wote ni Mtakatifu, uwe wa kimiujiza au ule uliosaidiwa na uwezo wa asili (natural means).
2. Kile kinachoitwa uponyaji wa kisasa (mtakatifu) sio mtakatifu wala sio uponyaji.
3. Sheria zote tuzitumiayo ni takatifu. Madaktari waligundua kwamba kwini ni maarufu kwa malaria, lakini ni nani aliyatengeneza lile gamba litumikalo kutengeneza dawa hiyo?
4. Si suala la nguvu ya Mungu? Angeweza kuzifanya karanga ziote kwenye mtikiti. Lakini ndivyo afanyavyo? Ni suala la sheria yake ni nini. Si jambo la nguvu bali ukweli.
5. Si suala la imani katika sala bali sheria ya Mungu kuhusu sala. Fikiria ningeomba (sali) kwa Mungu amfanye mtu kutokana na mavumbi ya nchi au mwanamke kutoka ubavu wa manamume, Je, Mungu angeyafanya hayo?

## II . Kwa nini miujiza ilitendeka.

1. Muujiza ni ishara au muhuri ambao Mungu anamkabidhi mwakilishi wake au kuuonyesha katika ufunuo wake (Mt. 9:2-8).
2. Kwanza ilianza miujiza kisha ikafuata sheria. Kufuatana na Adamu na hawa kulikuwa na sheria ya uumbaji na sheria ya uzazi. Sheria ya uzazi ni takatifu tu kama ilivyo sheria ya uumbaji. Kila mtoto huja duniani kutokana na sheria takatifu.
3. Miujiza ilikuwa ni nishani au ishara ya mamlaka, (Yn. 5:36, 14:11).

## III. Aina Tano za Miujiza.

1. Bwana anaonyesha nguvu yake juu ya sheria ya **asili**.
  - a) Mk. 4:39, "Upepo utulie". Pia Mt. 8:26.
  - b) Mt. 21:19 "Mtini kukauka."
2. Nguvu yake ilidhihirishwa juu ya **ugonjwa**.
  - a) Mt. 8:14,15, Alimponya mkwewe Petro.
  - b) Mt. 8:2-4, Mkoma aliponywa.
3. Alionyesha nguvu yake juu ya **mapepo**.
  - a) Mt. 18:16, Yesu alitoa mapepo.
  - b) Mt. 12:22, Mtu aliyeshikwa na pepo, kipofu na bubu aliponywa.
4. Yesu alidhihirisha nguvu juu ya vitu vya **kimwili**.
  - a) Mt. 14:15-21, wanaume elfu tano bila wana wake na watoto walishibishwa. Kwa mikate mitano na samaki wawilina mabaki kujaa vikapu 12.
  - b) Mt. 17:27 Yesu alimwambia Petro aende kuvua kwa ndoana wa kwanza kunaswa, mdomoni angekuwa na fedha ya kutosha kulipa kodi.
5. **Kifo** kilikomeshwa kwake mwishoni baada ya yeye mwenyewe kufufuka.
  - a) Alimfufua aliyekufa wakati wa utumishi wake, (Yn. 11:43).
  - b) Hata hivyo, ni baada ya kufufuka kwake, ndipo aliposema, "Ninayo mamlaka Mbinguni na duniani, (Mt. 28:18).

Kwa nini hawa watenda miujiza wanafanya miujiza miwili tu (ugonjwa na mapepo) kati ya aina hizo tano?

Kwa nini hawajaribu kufanya aina zote? **Ni dhahiri hawafanyi muujiza wo wote kati ya hiyo yote!**

#### **IV. Vipimo Vinne vya Roho.**

1. Yesu alipokea Roho pasipo kipimo, (Yn. 3:34).
2. Karama ya kawaida ya Roho, (Mdo. 2:38). “Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina la Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.”
3. Kipimo cha ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kilitolewa kwa mitume siku ya Pentekoste, (Mdo. 2) na wa karama hiyo hiyo kwenye nyumba ya Kornelio, (Mdo. 10).
4. Kulikuwa na karama maalum, (1 Kor. 12:4-11). Hizi karama tisa mtu alizipata kwa kuwekewa mikono: hekima, ufahamu, imani, uponyaji, kufanya miujiza, unabii, kupambanua Roho, aina za lugha na fasiri za lugha.

#### **V. Miujiza Iliendelea Mpaka Lini?**

1. Hawakuwa na Agano Jipya kamilifu wakati huo kwa sababu lilikuwa linatengenezwa.
2. 1 Kor. 12, Hutufahamisha idadi ya karama na, 1 Kor. 13 hutufahamisha muda (yaani kutumika mpaka lini).
3. 1 Kor. 12:31, “Takeni sana karama zilizo kuu, hata hivyo nawaonyesha njia iliyo bora.”
4. 1 Kor. 13:8, “Upendo haupungui neno wakati wo wote; bali ukiwepo unabii utabatilika; zikiwapo lugha zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika.”
5. Awali neno la Mungu lilikaa ndani ya mtu aliyevuviwa. Leo liko ndani ya kitabu kilichovuviwa. Paulo alisema, “Kwa maana tunafahamu kwa sehemu; na tunafanya unabii kwa sehemu; lakini ijapo ile iliyo kamili iliyo kwa sehemu itabatilika,” (1 Kor. 13:9, 10).

#### **VI. Hatimisho dhahiri.**

1. Miujiza ilikuwa ya muda tu. Katika uumbaji kulikuwa miujiza, kisha kukawa uzazi (sheria).
2. Miujiza ilikuwa ya lazima katika ufunuo (Biblia ilikuwa haijakamilika ) lakini si katika utangazaji. [Tunayanukulu ya miujiza yake].
3. Miujiza haikuwa ya kukaa bali likuwa maalum-kwa kusudi maalum-kwa muda maalum, kwa kipindi maalum.
  - a) Paulo alisema, “Trofimo nalimwacha huko Mileto, hawezi,” (2 Tim. 4:20). Kwa nini hakumponya? Alikuwa na uwezo.
  - b) Petro alifanya pigo kwa Anania na Safira akafa kutokana na kusema uongo, (Mdo 5).

Hicho ni kinyume kabisa cha uponyaji.
  - c) Paulo alifanya pigo kwa elima akapofuka, (Mdo. 13:10).

**Miujiza Hiyo Haiwezi Kurudiwa Rudiwa.**

**Uhudhurie Ibada za Kanisa la Kristo.**

**[www.kanisalakristo.com](http://www.kanisalakristo.com)**